# wakulima na matatizo ya masoko



TARP I

Varsha ya Nne ya
Vakulima wa Kanda ya
lyanda za Juu Kusini

iyofanyika Mjini Iringa,

arehe 6 – 8 Juni 2002

# MATATIZO YA MASOKO YA MAZAO YA WAKULIMA

**Warsha ya Nne ya Wakulima wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Iliyofanyika Kituo cha Anglikana, Iringa Juni 6-8, 2002**

**Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogo Wadogo Tanzania**
***(TARP II-SUA Project)***

**June 2002**

***Waandishi***

Bw. Razack O. Msangi
Prof. R. E. Malimbwi

***Wahariri***

Wajumbe wa kamati ya utekelezaji wa mradi:

| | |
|---|---|
| Prof. L. D. B. Kinabo - | Mratibu |
| Dk. Joyce G. Lyimo-Macha- | Mjumbe |
| Prof. E. K. Batamuzi - | Mjumbe |
| Prof. A. J. Tarimo - | Mjumbe |
| Dk. P. J. Makungu - | Mjumbe |

**ISBN: 9987 605 69 - 9**

*Kimechapishwa na:*

Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa
Wakulima Wadogo Wadogo Tanzania
(TARP II-SUA Project)
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo
SLP 3151
Morogoro
Simu: +255 23 2600970 au +255 23 2603511 ext. 4251

Toleo namba: TS2 - 52

# Yaliyomo

**Dibaji** .......... v
**Vifupisho** .......... vii

**1. UTANGULIZI** .......... 1
1.1 Madhumuni ya warsha .......... 1
1.2 Washiriki .......... 1
1.3 Ufunguzi .......... 1
1.4 Kushirikishana wajibu .......... 2

**2. MATARAJIO** .......... 2

**3. MBINU ZILIZOTUMIKA** .......... 3

**4. KUBAINI MATATIZO YA MASOKO** .......... 3
4.1 Makubaliano .......... 3
4.2 Kazi za vikundi .......... 4
4.2.1 Matatizo-wakulima .......... 4
4.2.2 Matatizo-Watafiti na Wagani/NGOs.......... 5
4.3 Tatizo kuu .......... 6

**5. MIKAKATI YA UTATUZI** .......... 7
5.1. Mikakati-Wakulima .......... 8
5.2. Mikakati-Watafiti.......... 9
5.3 Mikakati- Wagani .......... 10

**6. MATAMKO MUHIMU** .......... 11

**7. TATHMINI YA WARSHA** .......... 11

**8. KUFUNGA WARSHA**.......... 12

**9. VIAMBATANISHO** .......... 13

Kiambatanisho Namba A: Orodha ya washiriki .......... 13
Kiambatanisho Namba B: Ratiba ....... 15
Kiambatanisho Namba C: Zoezi18 .......... 16
Kiambatanisho Namba D: Dirisha la johari .......... 18

# Dibaji

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula, na Chuo Kikuu cha Norway cha Kilimo, kinatekeleza mradi wa Utafiti wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogo wadogo Tanzania. Mradi huu ambao ulianza rasmi mwezi Septemba 2000, unagharamiwa na Serikali ya Norway kupitia Shirika lake la Maendeleo (NORAD).

Kati ya shughuli muhimu zilizopangwa ili kutekeleza malengo ya mradi na kuimarisha uhusiano wa wakulima, watafiti na washauri wa wakulima ni kufanya warsha zenye madhumuni yafuatayo:

1. Kuwajumuisha watafiti, wakulima na washauri wa kilimo ili kudadisi kuhusu mambo muhimu yanayohitaji ushirikishwaji wa wadau wote kwa lengo la kufanikisha kilimo
2. Kuchambua na kuainisha matatizo yanayowakabili wakulima wadogo wadogo
3. Kupanga ili kutambua mambo gani yapewe uzito au kipaumbele zaidi
4. Kushiriki katika kupeana uzoefu wa maeneo muhimu ya kilimo.

Chapisho hili linawasilisha mwenendo wa Warsha ya Nne ya Wakulima wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Kuhusu Matatizo ya Masoko ya Mazao ya Wakulima, iliyofanyika katika ukumbi wa Kituo cha Anglikana, Iringa, tarehe 6-8 Juni 2002. Mwenendo wa warsha umechapishwa na kutolewa katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

L. D. B. Kinabo
Mratibu wa Mradi

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| COAS | Community Grassroot Initiatives Association *(Umoja wa Ushirikishwaji wa Jamii na Mipango)* |
| CBO | Community Based Organization *(Mashirika ya kijamii)* |
| MAFS | Ministry of Agriculture and Food Security *(Wizara ya Kilimo na Chakula)* |
| NGO | Non-Governmental Organization *(Shirika lisilo la Kiserikali).* |
| NLH | Chuo Kikuu cha Norway cha Kilimo. |
| SUA | Sokoine University of Agriculture *(Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo).* |
| TTCL | Tanzania Telecommunications Company Limited *(Shirika la Simu Tanzania)* |
| TARP II | Tanzania Agricutural Research Project Phase Two *(Mradi wa Taifa wa Utafiti wa Kilimo Awamu ya Pili)* |
| UNDP | United nations Development Programme *(Shirika la Umoja wa Mataifa la Mipango ya Maendeleo)* |

# UTANGULIZI

## *1.1 Madhumuni ya warsha*

Warsha iliandaliwa na Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania (TARP II-SUA Project) unaotekelezwa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula (MAFS) pamoja na Chuo Kikuu cha Norway cha Kilimo (NLH). Lengo kuu la warsha hiyo lilihusu kutazama kwa kina matatizo ya masoko ya mazao ya chakula yanayolimwa katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na kubuni njia mbalimbali ambazo zinnaweza kusaidia kuyatatua matatizo hayo. Kwa lengo hilo madhumuni mahususi ya warsha hiyo yalikuwa:

- Kubaini tatizo kuu na matatizo mengine yanayoambatana na tatizo kuu
- Kuainisha visababishi/viini vya matatizo hayo
- Kufikia mbinu muafaka (zilizo ndani na nje ya uwezo wa wadau) na kupendekeza wahusika wa utekelezaji wa mapendekezo hayo.

## *1.2 Washiriki*

Jumla ya washiriki 37 walihudhuria warsha hiyo ambayo ilifanyika katika Manispaa ya Iringa kituo cha mikutano cha Anglican. Washiriki 17 (ke 8 na me 9) walikuwa wakulima kutoka Wilaya za Sumbawanga, Songea, Iringa vijijini, Njombe, Mbeya vijijini, Mbozi, Mufindi, Mbarali na Namtumbo.

Washiriki watafiti 4 walitoka Taasisi ya cha Utafiti wa Kilimo Uyole, 6 walitoka SUA na mtafiti mmoja alitoka NLH Norway. Wagani wanne (4) walishiriki, na walitoka mikoa ya Mbeya, Iringa, Rukwa na Ruvuma. Kutoka ofisi ya kilimo ya Wilaya ya Iringa walikuwepo Afisa Kilimo na Afisa Mifungo wa Wilaya, Wagani wa Wilaya na Afisa Habari Uenezi. Kadhalika washiriki wawili walitoka mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) na mmoja kutoka COAS Iringa ndiye aliyekuwa mwezeshaji mkuu wa warsha (Kiambatanisho A).

## *1.3 Ufunguzi*

Katika ufunguzi wa warsha, Dk. (Bibi) Joyce Lyimo-Macha k.n.y mratibu wa mradi aliwakaribisha washiriki na kuelezea madhumuni ya warsha ambapo pia alibaini shughuli/malengo ya Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania (TARP II-SUA Project). Bibi Lyimo-Macha aliwaomba washiriki kujitambulisha kwa jina, wasifu na atokako. Baada ya utambulisho huo alimkaribisha mgeni rasmi Afisa Kilimo na Maendeleo ya Mifugo wa Wilaya ya Iringa vijijini, Dk. Nemes E.T. Makembe kufungua warsha.

Katika hotuba yake ya ufunguzi, mgeni rasmi aliwashukuru waandaaji wote waliowezesha warsha hii kufanyika hasa katika wakati huu ambapo uchumi wa nchi umetawaliwa na nguvu za soko na kwamba ilikuwa ni imani yake

kuwa kwa ujumla matokeo ya majadiliano ya washiriki yangechangia katika kuweka misingi endelevu ya kuwasaidia wakulima wadogo wadogo wa mazao ya chakula kanda ya Nyanda za Juu Kusini kuongeza kipato chao cha kaya na hivyo kupunguza umasikini. Mgeni rasmi aliwatahadharisha wakulima kuwa wauze mazao yao baada tu ya kujiwekea akiba ya kutosha ya chakula chao. Baada ya ufunguzi warsha iliendelea kwa kufuata ratiba (Kiambatanisho B).

### *1.4 Kushirikishana wajibu (responsibility sharing)*

#### *1.4.1 Viongozi wa warsha*

Kabla ya kuendelea na ratiba mwezeshaji alihamasisha washiriki kuchagua viongozi pamoja na kujiwekea kanuni. Bi Holiday A. Mwaisaka alichaguliwa kwa kura nyingi kuwa Mwenyekiti wa warsha akisaidiwa na Katibu Bw. Peter Ndakidemi. Kwa upande wa kuratibu masuala ya afya na lishe, Bi Fulgensia Nyenza na Bw. Sixberth Ndunguru walipewa jukumu hilo na Bw. Hassan Zayumba alichaguliwa kuwa mtunza muda.

#### *1.4.2 Kanuni*

Wanawarsha kwa pamoja walipanga kanuni kuu zifuatazo ambazo zilifuatwa na kila mshiriki wa warsha:

- Kutovuta sigara ukumbini/maeneo ya umma
- Kuzingatia na kutulia wakati wa kujadili mada
- Kujali na kuzingatia muda (muda ni mali)
- Kuthaminiana (kiumri, hoja, majibu, michango, n.k.)
- Kuheshimiana (kiumri, hoja, majibu, michango, n.k)
- Kuzingatia usafi wa mazingira
- Kutolewa darasani na katika maeneo ya hadhara
- Wote kuchangia kwa uwezo wote na uwazi
- Kushirikiana kama familia moja hadi mwisho wa warsha.

## 2. MATARAJIO

Wanawarsha walikuwa na matarajio yafuatayo:

- Kubaini matatizo yanayohusu masoko ya mazao ya chakula hususani yakiwemo mahindi na maharage, kupata mbinu za pamoja za kuyatatua matatizo hayo ili mkulima mdogo aweze kujikomboa kiuchumi kwa kuongeza kipato chake.
- Kukutana na kufahamiana na washikadau mbalimbali wa sekta hii, kuendelea kujenga mahusiano na watafiti, maafisa ugani, na wakulima na kubadilishana uzoefu wa namna ya kutatua matatizo mbalimbali kwa kutumia utafiti kutoka sehemu zingine.
- Kuelewa mikakati ya kitaifa kuhusu sekta ya kilimo, kupata ushauri kuhusu hifadhi ya mazao na mifugo.
- Kuelewa maana ya soko, aina ya mazao ya biashara Nyanda za Juu Kusini, na kuelewa namna ya kuanzisha ushirika wa kusimamia mazao ya wakulima wadogowadogo.
- Kufikisha mapendekezo Serikalini

Pamoja na matarajio hayo wanawarsha walionyesha wasiwasi kuhusu mafanikio ya warsha kwa vile mikutano/mikusanyiko kama hii imefanyika mara nyingi na maazimio kutolewa bila kuwa na utekelezaji au ushirikiano muafaka kutoka Serikalini, wadau mbalimbali na hata kutoka kwa wakulima wenyewe. Aidha, mazao ya chakula ni ya msimu, na kama mavuno ni haba kuna uwezekano uhamasishaji wa soko zuri kusababisha njaa kama wakulima hawatajiwekea akiba. Pia kulikuwa na wasiwasi kama mkulima ataweza kuhimili ujanja wa "walanguzi" wakati mitaji na karadha (credit) vijijini haipatikani na mazao kununuliwa kiholela holela bila vipimo maalumu ikiandamana na tatizo la kuwepo kwa vizuizi kadhaa vya kutoruhusu kuuza mazao hayo. Mjumuisho wa matarajio na hofu zilizoonyeshwa hapo juu vinaashiria kuwa washiriki wa warsha hiyo walielewa vyema maudhui (theme) ya warsha tokea majumbani kwao.

## 3. MBINU ZILIZOTUMIKA

Mbinu shirikishi zilitumika kwa kadiri ya uwezo wa kila mshiriki. Majadiliano yalifanyika katika vikundi vikubwa mchanganyiko, kadhalika ndani ya vikundi vidogo vidogo vilivyolenga watu/taaluma maalum, kwa mfano kundi la wanawake wakulima peke yao, wanaume wakulima peke yao, watafiti na wagani. Mbinu zingine zilitumika ni pamoja na kutoa maelekezo mafupi, majadiliano ya pamoja, chemsha bongo, washiriki kubadilishana uzoefu wa mifano hai ya kukabiliana na matatizo husika, vibwagizo vya kuondoa ukimya, michezo kadhaa ya kuongeza viwango vya ushirikishwaji ili kupanua ari ya kufikiri, kuchambua zaidi masuala mbalimbali pamoja na michoro iliyosaidia kueleweka kwa mada/hoja husika.

## 4. KUBAINI MATATIZO YA MASOKO

### *4.1. Makubaliano juu ya maana ya maneno ya msingi*

Kwa kuwa haja ya kujua maana ya baadhi ya maneno hayo hapo juu ilijitokeza kwenye matarajio ya wana warsha, muda wa kutosha ulitumika kueleweshana maana ya maneno ya msingi kama vile soko, sokoni, soko huria na tatizo/matatizo:

- **Soko** – ilikubalika kuwa ni taaluma inayohusu harakati au shughuli nzima za mzunguko wa bidhaa kutokea hifadhi, usafirishaji hadi uuzaji – (Soko ni fani/taaluma na sio mahali kama ilivyokuwa imefikiriwa na washiriki waliokuwa wengi).
- **Sokoni** – ilikubaliwa kuwa ni mahali ambapo zipo bidhaa/mazao/huduma ambapo wanunuzi na wauzaji hubadilishana bidhaa/huduma hiyo, kwa thamani watakayokubaliana.
- **Tatizo** (matatizo) – ilikubaliwa kuwa ni jambo/kitu chochote ambacho kinazuia. Maneno mbadala yaliyotajwa kulingana na maana hiyo ni pamoja na kigingi, kizingiti, kipingamizi au kizuizi
- **Soko huria** – ilieleweka kwa maneno kama kubabaisha, kutokuwa na uhakika, hali ya kuwepo kwa bei yoyote, hali ya kuuziana na kununua kwa bei ya makubaliano, hali ambayo wanunuzi hufuata bidhaa/mazao majumbani mwa watu ili wakanunue au wakauze. Kimsingi washiriki waliliona soko huria kama adui wa mkulima mdogo mdogo kama wakulima hawatajengewa uwezo wa kuelewa mazingira ya jinsi linavyofanya kazi ili waweze kuwa WASHINDANI

NA WAFANYA BIASHARA. Hivyo soko huria walielewa kuwa kumbe ni USHINDANI.

### *4.2 Kazi za vikundi ili kubaini matatizo na visababishi*

Washiriki walijigawa katika vikundi vinne; wanawake wakulima, wanaume wakulima, watafiti na wagani. Vikundi hivyo vilitumia muda wa kutosha kubaini matatizo ya masoko ya mazao ya chakula na sababu zake na kuwasilisha kwenye kundi kubwa ukumbini ambapo ufafanuzi na michango mbalimbali ilitolewa kukamilisha maelezo na muono wa kila kundi kama ifuatavyo: 4.2.1; majibu ya kundi la Wakulima (makundi mawili), na 4.2.2; majibu ya kundi la Watafiti na Wagani (makundi mawili).

### *4.2.1 Matatizo ya masoko ya mazao ya chakula na visababishi vyake (bila kujali kipaumbele) – kundi la Wakulima*

| WAKULIMA WANAWAKE | | WAKULIMA WANAUME | |
|---|---|---|---|
| **Matatizo kama walivyobaini (bila kujali kipaumbele)** | **Sababu zake kwa ujumla** | **Matatizo kama walivyobaini (bila kujali kipaumbele)** | **Sababu zake kwa ujumla** |
| 1. Kutokuwa na vyama vya ushirika vya kununua mazao.<br>2. Kutokuwa na bei ya kueleweka.<br>3. Wakulima kutokuwa na umoja wa kupanga bei na vipimo.<br>4. Vipo vizuizi mbalimbali wakati wa kuuza k.m. kutoruhusiwa kutoa/ kuuza mazao k.m. mahindi n.k. nje ya mkoa, nje ya nchi n.k.<br>5. Mitaji duni ya wakulima na kutomudu kununua mbolea na pembejeo zingine | • Ushindani si wa kweli, wanunuzi ni wachache.<br>• Ugumu wa maisha ya mkulima.<br>• Kutokushirikishwa wanawake wakati wa kuuza mazao (Utawala kwa mfumo dume katika jamii).<br>• Elimu duni ya wakulima walio wengi. | 1. Huduma duni (uwezo) wa wakulima wa kuhifadhi mazao yao ili wayauze kwa bei nzuri baadaye.<br>2. Kukosekana kwa Bodi ya kusimamia upangaji wa bei za awali/msingi kwa mazao ya chakula.<br>3. Ubora usiostahili wa mazao yapatikanayo, mbegu na pembejeo zingine (viwango vya ubora wa chini)<br>4. Kukosekana kwa ushirika wa kununua mazao na huduma zingine k.m. pembejeo n.k.<br>5. Kukosekana kwa mfumo sawia wa vipimo wakati wa kuuza.<br>6. Wakulima kuwa na elimu duni.<br>7. Ukosefu wa habari za masoko na wakulima kutokuwa na uwezo wa kuzichambua na kutumia habari hizo.<br>8. Uzalishaji duni utokanao na matumizi ya madawa, mbolea, na mbegu ambazo hazina viwango vinavyostahili.<br>9. Kukosekana kwa miundo mbinu muafaka vijijini k.m. madaraja na barabara, n.k. | • Umasikini wa wakulima kuongezeka.<br>• Ukosefu wa mitaji ya kutosha.<br>• Nyenzo duni za uzalishaji.<br>• Kuzama katika uzalishaji wa zao la aina moja. |

*4.2.2. Matatizo ya masoko ya mazao ya chakula na visababishi vyake - kundi la Watafiti na Wagani*

| WATAFITI | | WAGANI | |
|---|---|---|---|
| **Matatizo kama walivyobaini (bila kujali kipaumbele)** | **Sababu zake** | **Matatizo kama walivyobaini (bila kujali kipaumbele)** | **Sababu zake** |
| 1. Bei ndogo ya mazao ikilinganishwa na bei kubwa ya pembejeo<br>2. Serikali kuingiza mazao/chakula kutoka nje hivyo kuathiri soko la ndani<br>3. Ukosefu wa taarifa za masoko kwa mazao ya chakula<br>4. Uzalishaji usio endelevu wa mazaao ya chakula ambao hautoi ziada ya kuuza.<br>5. Watafiti kutotafiti kwa wakati muafaka athari za madawa pembejeo bandia ziingizwazo sasa, na pia athari za kuuza au kutouza mazao ya chakula nje ya mipaka ya nchi. | • Wakulima kutokuwa na uwezo wa kudhibiti bei ya mazao katika soko huria.<br>• Pembejeo zinaagizwa toka nje hivyo bei kuwa juu<br>• Kukosa chombo cha kuwaunganisha wakulima wadogo wadogo kuamua pamoja<br>• Serikali kuondoa ruzuku kwenye pembejeo<br>• Bidhaa/mazao kukosa ubora wa kuuzika kwa bei nzuri<br>• Mkulima kulazimika kuuza kwa bei yoyote kutokana na matatizo aliyonayo<br>• Kutokuwa na elimu (ujuzi) ya usindikaji wa mazao<br>• Kutokuwa na taarifa za bei ya mazao kutoka sehemu mbalimbali<br>• Mkulima kuwa na uwezo mdogo wa miundo mbinu ya kuhifadhi mazao<br>• Serikali kutokuwa na takwimu za uhakika juu ya upungufu wa chakula nchini<br>• Mfumo mbovu wa taarifa za masoko (kitengo kipo Wizarani tu, Mikoani, Wilayani, tarafani hakuna)<br>• Hali mbaya ya hewa<br>• Utumiaji wa pembejeo zisizokidhi viwango (below standards) | 1. Hakuna soko la uhakika na uzalishaji ni mdogo<br>2. Kupanuka kwa maeneo ya uzalishaji kwa aina chache za mazao (mahindi, mpunga)<br>3. Vizuizi vya serikali, kodi nyingi kwa mazao husika na kutoruhusiwa kuuza nje ya mipaka<br>4. Ukosefu wa taarifa za masoko na udhaifu wa wakulima kuchanganua na kutumia taarifa hizo<br>5. Ubora finyu wa mazao yanayozalishwa<br>6. Wakulima kutotumia elimu/utaalamu wa kilimo uchumi - hawaweki kumbukumbu za gharama zao za uzalishaji n.k.<br>7. Wakulima kukosa elimu/taaluma ya usindikaji wa mazao. | • Udhaifu wa sera za soko huria<br>• Hakuna chombo cha kutetea/masoko/ maslahi ya wakulima<br>• Umasikini na ukosefu wa mitaji kwa wakulima<br>• Uvivu na uzembe wa wadau mbalimbali<br>• Matumizi ya nyenzo duni<br>• Wakulima kutegemea zaidi zao moja<br>• Sera na sheria mbalimbaali zinaathiri<br>• Matukio ya rushwa "kitengo cha SGR hakimthamini mkulima mdogo ambaye hawezi "KURUKA" hasa wakati wa kuuza mahindi yao<br>• Udhaifu wa kitengo cha masoko kilichopo wizarani tu<br>• Wakulima kutotumia mbinu bora za kilimo<br>• Ubovu wa miundo mbinu vijijini (barabara n.k.)<br>• Uchache wa watumishi ugani na kupangiwa kazi za "kodi" zisizokuwa zao.<br>• Umasikini wa jamii na elimu duni<br>• Hali ya hewa na jiografia ya maeneo mengine huruhusu zao la aina moja tu.<br>(KURUKA=kutoa rushwa) |

### *4.3 Tatizo kuu na maeneo ya kumsaidia mkulima:-*

Baada ya kila kikundi kumaliza kuwasilisha na kutetea/kuongeza yale yaliyolenga kuboresha kazi za kila kikundi, takribani washiriki wote walikuwa na sura bashasha jioni ya siku ya pili kwa kuanza kuamini kuwa matatizo, sababu na namna ya kuanza kutafuta ufumbuzi wa matatizo yanayo wakabili yalikuwa yanajionyesha vizuri zaidi. Tathmini ya siku ya pili jioni ilionyesha hivyo – washiriki wengi walitamka hivyo.

Kwa sababu hiyo, mwezeshaji alichangia na kufanya majumuisho ya matatizo husika kwa ujumla, kama ifuatavyo:

**Tatizo kuu la masoko ya mazao ya chakula kwa mkulima ni kukosekana kwa hali ya wakulima kujirekebisha na kujipanga ipasavyo ili kuhimili mikiki ya soko huria**. Kwa sababu hiyo wakulima/wazalishaji wadogo wadogo wa mazao ya chakula wanakosa mfumo wao wa pamoja na uamuzi wa pamoja wa kupanga bei ya mazao yao, n.k. Hali hii ya wakulima kutoona pamoja inawafanya wawe wateja wa "wajanja" wa soko huria na wapangiwe bei isiyolipa gharama zao za uzalishaji, wauziwe pembejeo, madawa yasiyofaa na hivyo kushindwa kufanya biashara kama inavyotazamiwa kwenye mfumo wa soko huria. Hivyo wakulima wanabakia kulima na kuuza kwa watu mbalimbali ambao watu hao hutumia fursa nzuri za soko huria na mianya kadha wa kadha kuendelea kumpunja mkulima wakati yumkini wao huendelea kunufaika kibiashara.

Matokeo ya hali na uhusiano huo ni mkulima kuendelea kuathirika kama ifuatavyo:-

- ***Bei*** – ya mazao yake huendelea kuwa ndogo ikilinganishwa na gharama za uzalishaji (aghalabu wakulima wengi hawazijui gharama zao za uzalishaji). Wakati huo huo bei za zana, madawa na pembejeo za kilimo ni kubwa.
- ***Ubora***- Ubora wa mazao yenyewe ni wa chini na dawa na pembejeo zitumikazo zipo chini ya viwango.
- ***Sera/sheria*** – Baadhi ya sera na sheria zilizopo hazimlindi mkulima mdogo. Kodi kadha wa kadha zimeambatana na mazao ya chakula na utaratibu uliokusudiwa kurahisisha maendeleo/kukua kwa soko huria unawekewa ukiritimba/vikwazo. Wawekezaji hawajapata mvuto wa kuwekeza kwenye sekta ya kilimo pamoja na usindikaji wa mazao ya chakula.
- ***Ubovu wa miundo mbinu*** – Jukumu la kudumisha barabara za vijijini kiwango cha kupitika mwaka mzima bado linahitaji juhudi kubwa. Wakulima wangeweza kutengeneza maeneo husika kurahisisha usafirishaji wa mazao yao; lakini bado majukumu makubwa ni ya Halmashauri za Wilaya na Serikali Kuu.
- ***Ukosefu na uduni wa matumizi ya habari za masoko*** – Ni vyema jitihada zikafanyika kupanua huduma hizi kutoka kitengo kinachohusika Makao Makuu ya Wizara ya Ushirika na Masoko, kuja Mikoani hadi Wilayani n.k. Vivyo hivyo Wagani husika wa Mikoa na Wilaya wangeweza kuanzisha "marketing

information systems" (MIS) zao msimu kwa msimu Kimkoa au Kiwilaya, Kikata n.k.

- ***Kukosa soko la uhakika na uzalishaji mdogo*** – Haya yote ni matokeo ya matumizi ya mbegu duni, mbolea za kughushi"feki", matumizi ya zana duni za kilimo, kutotumia utaalamu wa kilimo, kutotumia kilimo asilia, hifadhi mbovu ya mazingira (mmomonyoko wa udongo) n.k.
- ***Wakulima kutokuwa na mifumo yao*** – Mifumo hiyo ikiundwa na kuendelezwa (mifano ya Producer Marketing Groups (PMGs) za Iringa, vikundi vya uzalishaji na uuzaji wa mpunga Chimala Mbeya na kikundi cha uuzaji wa mahindi – Kibaigwa Dodoma vilitajwa) itasaidia kupanga bei ya mazao ya kikundi/wakulima husika, kuweka viwango muafaka wa vipimo (ujazo/uzito), kuamini uongozi wao wa pamoja na kuheshimu uamuzi wao wa pamoja, na mara kwa mara hufanikiwa kwa kuwa mtazamo wao huwa ni wa kibiashara (wakulima wafanyabiashara).
- ***Ukosefu wa mitaji*** – Kukosa namna ya kujipanga ili waanzishe mifuko yao ya ndani.
- ***Kutofahamika/kutotangazika vyema***
- ***Wimbi la kutakiwa kutoa chochote*** - "kuruka" ili kupata haki yao. Kitengo cha Taifa cha Hifadhi ya Akiba ya chakula (SGR) kilitajwa sana na washiriki "kuwa watendaji wake ni wapenda rushwa"

Wanawarsha walikubaliana kuanza kujenga tabia ya kukataa kutoa "chochote" (rushwa) kwa huduma yoyote ambayo ni haki yao.

Kadhalika maeneo yafuatayo yalibainishwa na kukubalika na wanawarsha kuwa ndiyo maeneo makuu ya kuanza kumsaidia mkulima:-

(1) Wasaidiwe kupata wanunuzi wa mazao mbalimbali
(2) Wasaidiwe kupata na kutumia habari za masoko pamoja na kubaini mazao mbadala kufuatana na hali halisi ya soko
(3) Wasaidiwe kujengewa uwezo wa kuwa na mifumo yao (organisational skills) na kufikia uamuzi– (lini, vipi, kiasi na ubora wa kuuza)
(4) Wasaidiwe kutambua njia mbalimbali za kuboresha masoko yao – kwa mfano wawezeshwe kuelewa mfumo wa soko huria unavyofanya kazi (warsha hii ikiwa njia sahihi ya kuianza kazi hiyo)
(5) Wasaidiwe kudumisha miundo mbinu – barabara bora, hifadhi ya mazao n.k.
(6) Wasaidiwe kubuni na kukuza mitaji endelevu

## 5.0 MIKAKATI YA UTATUZI WA MATATIZO NA KUASHIRIA WAHUSIKA

Wanawarsha walijigawa katika makundi makuu manne (4) ya Wagani, Watafiti na Wakulima (mchanganyiko – makundi 2), ili kupanga mikakati husika na kuashiria watekelezaji kama inavyoonyeshwa katika jedwali 4.1 na 4.2.

5.1 *Mikakati/mapendekezo ya kutatua matatizo na watekelezaji wakuu (wahusika) kundi la wakulima.*

| | MIKAKATI/MAPENDEKEZO | WAHUSIKA WAKUU |
|---|---|---|
| 1. | **Wakulima wasaidiwe kupata wanunuzi:** | |
| | 1.1. Wakulima wenyewe wajiwekee mikakati ya kuunda vikundi vyao wenyewe vya kudhibiti bei za mazao yao na vipimo ndani ya soko huria (Mifano ya PMGs za Iringa, Kibaigwa – Dodoma na Chimala – Mbeya vilitajwa kama mbinu sahihi.) | 1.1. Wakulima wenyewe – na viundwe mapema iwezekanavyo |
| | 1.2. Serikali isaidie kutafuta masoko ndani na nje ya nchi k.m. kwa kutumia nafuu za AGOA, EAC, SADC n.k. | 1.2. Serikali ngazi zote sasa na baadaye (short, medium & long term) |
| 2. | **Kupata na kutumia habari za masoko:** | |
| | 2.1. Wakulima wawe mstari wa mbele kuunda chombo ambacho kitawaunganisha wote kwa ajili ya mawasiliano na habari za masoko. | 2.1. Wakulima wenyewe – kuanzia sasa waanze KUFURUKUTA katika kila Mkoa. SUA na Taasisi za utafiti zisaidie kuunganisha juhudi hizi kupitia mradi wa TARP II –SUA Project. |
| | 2.2. Kujenga mahusiano mazuri kuanzia ngazi ya mkulima na mkulima, Kijiji na Kijiji, Wilaya na Wilaya, Mkoa hatimaye Taifa. | 2.2. Wakulima na Serikali za ngazi zote. Mwanzo uwe ni wakulima, Serikali za Vijiji na zile za halmashauri za Wilaya |
| | 2.3. Kuweka utaratibu wa kufuatilia na kupata habari husika za masoko | 2.3. Wakulima, Watafiti na Wagani |
| 3. | **Kufikia uamuzi wa lini, vipi, kiasi na ubora** | |
| | 3.1. Ndani ya umoja wao/mshikamano wao, wakulima wajipangie mikakati bora ya kuzalisha mazao mbalimbali na yawe bora, kadhalika wajijengee uwezo wa kupanga kiasi cha kuuzwa kwa kufuata mahitaji na nguvu za soko. | 3.1. Wakulima wenyewe na mitandao/ vikundi vyao. |
| | 3.2. Serikali isimamie vizuri na kudhibiti utekelezaji wa sera za soko huria (regulatory function) | 3.2. Serikali za Wilaya na Serikali Kuu. |
| 4. | **Kuboresha njia mbalimbali za masoko** | |
| | 4.1. Wakulima wahakikishe wanadumu ndani ya mkakati wa kuwa na sauti ya pamoja katika kupanga bei za mazao yao | 4.1. Wakulima wenyewe na sasa waanze kufurukuta kote nchini |
| | 4.2. Kujenga uhusiano wa karibu na wagani pamoja na watafiti waliopo na kuwa wakulima wafanya biashara. | 4.2. Wakulima, Wagani, Watafiti na Serikali za Vijiji na za Wilaya. |
| | 4.3. Serikali inapounda sera zihusuzo matatizo au manufaa ya wakulima, sera hizo ziwe na mfumo shirikishi kwa kuanzia ngazi za chini hadi Taifa | 4.3. Serikali za Vijiji, Wilaya na Kuu serikali kuu |

| | | |
|---|---|---|
| 5. | **Kudumisha miundo mbinu**<br>5.1. Wakulima washirikishwe kubuni na kuendeleza miundo mbinu ndani ya umoja wao (kwa wale ambao tayari wanao) na ule utakaoanzishwa. Mifano iwe katika ujenzi wa barabara ili kuwavutia wawekezaji na wanunuzi.<br>5.2. Serikali isaidie kuimarisha miundo mbinu inayoanzishwa na wakulima au iliyoanzishwa na Serikali yenyewe k.m. TASAF | 5.1. Wakulima wenyewe<br><br>5.2. Serikali za vijiji, Halmashauri na serikali kuu. |
| 6. | **Kubuni na kukuza mitaji endelevu**<br>6.1. Wakulima kujiunga na vyama au vikundi vya Akiba na Mikopo (SACCOs na SACCAs) ili kuinua na kuimarisha mitaji yao kwa kukopeshana wao wenyewe badala ya kutegemea misaada tu.<br>6.2. Serikali itoe ruzuku katika vyama/vikundi hivyo vya Akiba na Mikopo ili kuviimarisha kiuchumi. | 6.1. Wakulima wenyewe<br><br>6.2 Halmashauri za Wilaya zianze na baadaye Serikali Kuu. |

### 5.2 *Mikakati/mapendekezo ya kutatua matatizo na watekelezaji wakuu (wahusika) kundi la watafiti*

| | MIKAKATI/MAPENDEKEZO | WAHUSIKA |
|---|---|---|
| 1. | ***Tatizo***: Wakulima kukosa mifumo yao.<br>***Utatuzi***: (i)Wakulima washirikiane waweze kuwa na sauti na maamuzi ya pamoja kuhusu soko la mazao yao | (i) Wakulima na wagani mapema iwezekanavyo |
| 2 | ***Tatizo***: Kutokuwa na soko la uhakika; bei ndogo.<br>***Utatuzi: (i)***Vikwazo/vizuizi vya kuuza mazao ndani na nje ya nchi viondolewe. Wakulima walime kisasa na kuzingatia ubora.<br>(ii) Watafiti watafute athari za "free border trading" na vizuizi vingine.<br>- Gunia moja la kg 120 za mahindi Songea ni Shs. 4,000/=, Msumbiji Shs. 36,000=.<br>- Gunia moja la kgs 120 za mahindi Rukwa 6,000/=, Zambia 18,000/= [1]<br>(iii) Wakulima waelimishwe njia mbalimbali za kutambua na kuboresha masoko | (i) Wakulima na watafiti mapema iwezekanavyo<br>(ii) Watafiti Serikali za Wilaya na Serikali Kuu zitoe ushirikiano<br><br>(iii) Wakulima, wagani mapema iwezekanavyo |
| 3 | ***Tatizo***: Ubovu wa miundo mbinu<br>***Utatuzi***: Wakulima wahamasishwe na kuhamasishana kudumisha miundo mbinu iliyopo – kuwezesha soko la mazao | Wagani na wakulima mapema, iwezekanavyo |

[1] (Chanzo : washiriki wa warsha – 7/06/2002 Iringa)

### 5.3 *Mikakati/mapendekezo ya kutatua matatizo na watekelezaji wakuu (wahusika) kundi la wagani*

| | MIKAKATI/ MAPENDEKEZO | WAHUSIKA |
|---|---|---|
| 1 | *Tatizo*: Bei ndogo ya mazao na bei kubwa ya pembejeo<br>*Ufumbuzi:* | |
| | (i) Kuanzisha/ kuimarisha umoja wa wakulima | (i) NGOS, wakulima wanunuzi (Buyers) |
| | (ii) Kulima kwa mkataba | (ii) Wakulima na wagani na NGOs |
| | (iii) Matumizi sahihi ya mbolea na madawa asili | (iii)Wakulima, wagani na NGOs |
| | (iv) Ruzuku ya pembejeo kwa wakulima irejeshwe (Marekani wanawapa ruzuku ya 60% wakulima wao!) | (iv) Serikali Kuu |
| | (v) Kuanzisha/kuimarisha taasisi za kifedha vijijini | (v) Wakulima, NGOs na Taasisi za kifedha |
| | (vi) Kuondoa vizuizi visivyofaa na kufungua mipaka na majirani inapobidi. | (vi) Serikali za ngazi zote |
| | (vii) Kuanzishwa kwa chombo (bodi) ya nafaka itakayosimamiwa na kuendeshwa na wakulima wenyewe (National Grain Board) | (vii) Wakulima na Serikali kusaidia |
| 2 | *Tatizo*: Ubora hafifu wa mazao na pembejeo<br>*Ufumbuzi*: | |
| | (i) Kuboresha mbinu za uzalishaji na | (i) Wakulima na wagani |
| | (ii) Kudhibiti uingizaji na uuzaji wa pembejeo na madawa yasiyotimia viwango | (ii) Watafiti, wagani na Serikali za ngazi zote. |
| | (iii) Wakulima watilie mkazo matumizi sahihi ya mbolea na madawa asilia | (iii)Wakulima na wagani |
| 3 | *Tatizo*: Sera na sheria zinaathiri masoko<br>*Ufumbuzi*: | |
| | (i) Kupungua/kundoa baadhi ya kodi kwa wakulima | (i) Serikali kuu na za Wilaya |
| | (ii) Kuondoa ukiritimba, k.m. vizuizi barabarani | (ii) Serikali za vijiji na Wilaya |
| | (iii)Usimamizi wenye ufanisi wa sera ziwe shirikishi | (iii)Serikali za ngazi zote. |
| 4 | *Tatizo*: Ubovu wa miundo mbinu<br>*Ufumbuzi:* Miundo mbinu (usafirishaji, hifadhi n.k.) iimarishwe. | Wakulima, Serikali za ngazi zote na wafanyabiashara. |
| 5 | *Tatizo:* Ukosefu na kutotumia habari za masoko<br>*Ufumbuzi:* | |
| | (i) Kitengo cha masoko Wizara ya Ushirika na Masoko kiimarishwe hadi vijijini | (i) Serikali Kuu hadi za Wilaya |
| | (ii) Wakulima na vyombo vyao kufuatia habari za masoko ya mazao. | (ii) Wakulima na umoja wao (vyombo vyao) |
| 6 | *Tatizo*: Ukosefu wa Mitaji<br>*Ufumbuzi* | (i) Serikali, mifuko husika, na NGOs |
| | (i) Wakulima wasaidiwe mitaji kutokana na mafungu/ mifuko ya umma/jamii k.m. TASAF n.k. | (ii) Wakulima NGOs/ CBOs |
| | (ii) Wakulima kuanzisha mifuko yao ya ndani ya mazao, pembejeo, uendeshaji n.k. | (iii) Wakulima, wagani na NGOs/ CBOs |

| | | |
|---|---|---|
| | (iii) Wakulima wahamasishwe kuanzisha vyombo vyao vya Akiba na Mikopo na waendeleze tabia ya kujiwekea akiba mara kwa mara. | |
| 7 | ***Tatizo***: Wakulima kutokuwa na mfumo wao wa uendeshaji na kukosa kujitangaza (kufahamika)<br>***Ufumbuzi***: Wakulima waanzishe na kuimarisha vikundi (vyombo) vyao vitakavyoweza kupanga bei, kutunza kumbukumbu mbalimbali za uzalishaji, kudhibiti vipimo, kuhamasisha uzalishaji bora, n.k. | Wakulima, wagani na NGO's. |

## 6. MATAMKO MUHIMU YA WARSHA

1. Warsha ilitamka kuwa matokeo ya kazi ya warsha hii ya kuchambua matatizo ya masoko ya mazao ya wakulima iwafikie watendaji Wakuu wa Wizara za Kilimo na Chakula, Ushirika na Masoko, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa hatua za utekelezaji. Aidha, vikwazo/vizuizi vilivyopo vinavyomzuia mkulima kuuza mazao yake ya ziada kwa mfumo wa soko huria kivitendo vilegezwe au vipunguzwe na kuondolewa kabisa pale itakapobidi.
2. Warsha kama hii zitumike na Serikali na wadau wengine ili kupata maoni ya wakulima wananchi wakati wa kuandaa sera na mikakati inayowagusa katika maisha yao ya kila siku.
3. Jitihada zichukuliwe ili hapo baadaye warsha kama hii ifanyike kwa ajili ya kupima utekelezaji.

## 7. TATHMINI YA WARSHA

Tathimini ya warsha ilifanyika kwa kila mshiriki kuandika maoni yake katika kadi tatu, moja akieleza ni imani gani ameijenga baada ya kuja, kuona, kusikia na kushiriki katika warsha hii. Kadi ya pili, mambo ambayo hayakumridhisha na maoni ya namna ya kuyaboresha na ya tatu, juu ya maandalizi na mbinu zilizotumika katika uwezeshaji. Matokeo ya tathmini yameonyeshwa katika jedwali 7.1.

## 9. VIAMBATANISHO

## KIAMBATANISHO A: ORODHA NA ANUANI ZA WASHIRIKI

| Na. | Jina | Jinsia | Kazi | Kijiji | Kata | Anuani |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Gaudensia V. Mavazi | Ke | Mkulima | Katumba/Azimio | Pito | S. L. P. 170 Sumbawanga |
| 2. | Peter G. Ngonyani | Me | Mkulima | Peramiho | Maposeni | S. L. P. 14 Peramiho, Ruvuma |
| 3. | Iva Lusasi | Me | Mkulima | Magulilwa | Magulilwa | C/O Nyabula Parish Mission<br>S. L. P. 170 Iringa |
| 4. | Fulgensia N. Nyenza | Ke | Mkulima | Makungugu | Nduli | ARI Uyole (Isimani Substation)<br>S. L. P. 340 Iringa |
| 5. | Mariana K. Mlelwa | Ke | Mkulima | Madaba | Mahanje | S. L. P. 3 Madaba, Songea |
| 6. | Zawadi Mbingalala | Ke | Mkulima | Ruaha/Mbuyuni | Mtandika | S. L. P. 280 Iringa |
| 7. | Agnes J. Mlowe | Ke | Mkulima | Ibumila | Igongolo | S. L. P. 323 Njombe, Iringa |
| 8. | Desdery C. Lupamba | Me | Mkulima | Matai | Matai | S. L. P. 229 Sumbawanga |
| 9. | Ruth S. Mwangosi | Ke | Mkulima | Idiga | Songwe | S. L. P. 4960 Mbeya |
| 10. | Peter Mwanandenje | Me | Mkulima | Isesa | Isesa | S. L. P. 223 Sumbawanga |
| 11. | Joseph J. Mwampashi | Me | Mkulima | Ivwanga | Mlowa | Shule ya Msingi Ivwanga<br>S. L. P. 277 Mbozi, Mbeya |
| 12. | Habakuki S. Nsyenge | Me | Mkulima | Sao Hill | Mafinga | S. L. P. 176 Mafinga |
| 13. | Issabela Newa | Ke | Mkulima | Lumecha | Msindo | S. L. P. 960 Songea, Ruvuma |
| 14. | Hebel M. Mwanisisi | Me | Mkulima | Iwindi | Iwindi | Iwindi Moravian Church<br>S. L. P. 1190 Mbeya |
| 15. | Lugano W. Mwandenga | Me | Mkulima | Chimala | Chimala | S. L. P. 78 Chimala-Mbarali |
| 16. | Fadhili M. Kitete | Me | Mkulima | Namtumbo | Namtumbo | S. L. P. 02 Namtumbo, Songea |
| 17. | Mary Seketea | Ke | Mkulima | Mbuza | Mkowe | S. L. P. 229 Sumbawanga |
| 18. | Sixberth N. Ndunguru | Me | Mgani (VEO) | Lilondo | Wino | S. L. P. 174 Songea, Ruvuma |
| 19. | Nictor Y. Ngusi | Me | Mgani (VEO) | Matai | Matai | Kilimo Wilaya<br>S. L. P. 232 Sumbawanga |
| 20. | Hassan J. M. S. Zayumba | Me | Mgani (VEO) | Idodi | Idodi | S. L. P. 290 Iringa |
| 21. | Peter J. Ndakidemi | Me | Mgani (VEO) | Chimala | Chimala | S. L. P. 141 Chimala |
| 22. | Meshack J. Mbogollo | Me | Mtafiti | ARI Uyole | ARI Uyole | ARI Uyole<br>S. L. P. 400 Mbeya |
| 23. | Anthony M. Elanga | Me | Mtafiti | ARI Uyole | ARI Uyole | ARI Uyole<br>S. L. P. 400 Mbeya |
| 24. | Zacharia J. U. Malley | Me | Mtafiti | ARI Uyole | ARI Uyole | ARI Uyole<br>S. L. P. 400 Mbeya |
| 25. | Dorothy Machunda Gimbi | Ke | Mtafiti | SUA | SUA | Idara ya Sayansi ya Chakula<br>S.L.P. 3006 Morogoro |
| 26. | Ephraim M. M. Senkondo | Me | Mtafiti | SUA | SUA | S. L. P. 3007 Morogoro |
| 27. | Nemes E. T. Makembe | Me | DALDO | Iringa | Iringa | S. L. P. 290 Iringa |
| 28 | Holiday A. Mwakasaka | Ke | NGO | Lizaboni | Lizaboni | S. L. P. 268 Songea |
| 29 | Filemon B. Mpwehwe | Me | DEO | Iringa | Iringa | S. L. P. 290 Iringa |
| 30 | Emil M. P. Kissoka | Me | Afisa Habari | Iringa | Iringa | Kitengo cha Habari (Uenezi)<br>S. L. P. 389 Iringa |
| 31 | Grete Benjaminsen | Ke | Mtafiti | ÅS Norway | ÅS Norway | S.L. P. 5001 Noragric, NLH |

## JEDWALI 7.1 TATHMINI YA WARSHA

| Fungu kubwa (Cluster No.) | SWALI LA KWANZA<br>Baada ya Warsha Imani iliyojengeka (Clustered opinions) (Maoni) | Idadi ya washiriki |
|---|---|---|
| 1. | Lazima wakulima tukajipange upya na kuanza kufurukuta, hakuna lisilowezekana. Wakullima tunaweza kubadilika kwa haraka zaidi kwa kujiunga na kushirikiana pamoja kutafuta soko zuri. Haja ya kuunda vikundi vya mshikamano ni nyeti kwani vikundi vitasaidia kutatua baadhi ya matatizo ya ukosefu wa masoko na bei ndogo ya mazao. Kadhalika matokeo yake ni kwamba pato la kaya na uhakika wa chakula litafanikiwa kwani utaalamu wa kilimo cha kisasa utatumika. Mikakati tuliyojiwekea ikitekelezwa ipasavyo na kila mhusika, matatizo mengi yanayohusu soko la mazao ya chakula yatapungua au kwisha kabisa. | 30 |
| 2. | Ushirikishwaji wa wadau katika kutatua matatizo yao ni kitu muhimu sana, hivyo makongamano ya wakulima ni ya muhimu. Nimejifunza mengi yanayohusu maendeleo ya maisha na naamini kuwa mabadiliko yanaanzia kwa mtu mmoja, mabadiliko ni vita hivyo tupambane. Ushirikishwaji na uhamasishaji ukiwa na ufanisi, wakulima wanaweza kutatua matatizo yao hata yakiwa magumu kiasi gani. Yaliyoonekana, kusikiwa na kushiriki ndiyo yatakuwa dira kubwa ya kuleta mabadiliko. | 10 |

| Fungu kubwa (Cluster No.) | SWALI LA PILI<br>Ambayo hayakuniridhisha na namna ya kuboresha (Clustered opinions) | Idadi ya washiriki |
|---|---|---|
| 1. | Hayakuwepo ambayo hayakuridhisha | 18 |
| 2. | Fursa ya kuchagua chakula iwepo, lugha zisichanganywe, taarifa za warsha na mabadiliko yoyote yale ziwe za muda wa kutosha | 5 |
| 3. | Muda wa warsha uongezwe na kazi kwa vikundi wachanganye watafiti, wagani na wakulima na mazoezi (vibwagizo) vingine vizingatie mila na desturi k.m. lile zoezi la kupeana migongo | 4 |
| 4. | Je inawezekana kuwaita watu hawa hapo baadae ili kupima utekelezaji? Baada ya miezi sita tukutane na kuona utekelezaji wa tunakokwenda. | 2 |

| Fungu kubwa (Cluster No.) | SWALI LA TATU<br>Maoni kuhusu maandalizi na mbinu zilizotumika katika uwezeshaji (Clustered opinions) | Idadi ya washiriki |
|---|---|---|
| 1. | Maandalizi mazuri na mbinu za uwezeshaji zilizotumika ni nzuri, ni mbinu shirikishi na rahisi kuelewa. Mwezeshaji ametimiza wajibu wake ipasavyo, suala la jinsia limeangaliwa, mbinu zidumu tena na tena, tunashukuru sana kwa mambo yote. | 18 |
| 2. | Katika kuchangia mada, nafasi nyingi wapewe wakulima, wanapokuwa wazito wachokozwe kwa kutajwa majina ili kusiwe na wachache wanaotawala mjadala. | 3 |

## 8. KUFUNGA WARSHA

Warsha ilifungwa rasmi na Katibu Tawala wa Mkoa wa Iringa kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Iringa Meja Jenerali James Luhanga. Pamoja na ufungaji huo, washindi wa mashindano ya wakulima, wagani na watafiti katika Kanda ya Nyanda za Juu Kusini walitunukiwa zawadi za vyeti vya utendaji bora pamoja na fedha taslimu.

# 9. VIAMBATANISHO

## KIAMBATANISHO A: ORODHA NA ANUANI ZA WASHIRIKI

| Na. | Jina | Jinsia | Kazi | Kijiji | Kata | Anuani |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Gaudensia V. Mavazi | Ke | Mkulima | Katumba/Azimio | Pito | S. L. P. 170 Sumbawanga |
| 2. | Peter G. Ngonyani | Me | Mkulima | Peramiho | Maposeni | S. L. P. 14 Peramiho, Ruvuma |
| 3. | Iva Lusasi | Me | Mkulima | Magulilwa | Magulilwa | C/O Nyabula Parish Mission<br>S. L. P. 170 Iringa |
| 4. | Fulgensia N. Nyenza | Ke | Mkulima | Makungugu | Nduli | ARI Uyole (Isimani Substation)<br>S. L. P. 340 Iringa |
| 5. | Mariana K. Mlelwa | Ke | Mkulima | Madaba | Mahanje | S. L. P. 3 Madaba, Songea |
| 6. | Zawadi Mbingalala | Ke | Mkulima | Ruaha/Mbuyuni | Mtandika | S. L. P. 280 Iringa |
| 7. | Agnes J. Mlowe | Ke | Mkulima | Ibumila | Igongolo | S. L. P. 323 Njombe, Iringa |
| 8. | Desdery C. Lupamba | Me | Mkulima | Matai | Matai | S. L. P. 229 Sumbawanga |
| 9. | Ruth S. Mwangosi | Ke | Mkulima | Idiga | Songwe | S. L. P. 4960 Mbeya |
| 10. | Peter Mwanandenje | Me | Mkulima | Isesa | Isesa | S. L. P. 223 Sumbawanga |
| 11. | Joseph J. Mwampashi | Me | Mkulima | Ivwanga | Mlowa | Shule ya Msingi Ivwanga<br>S. L. P. 277 Mbozi, Mbeya |
| 12. | Habakuki S. Nsyenge | Me | Mkulima | Sao Hill | Mafinga | S. L. P. 176 Mafinga |
| 13. | Issabela Newa | Ke | Mkulima | Lumecha | Msindo | S. L. P. 960 Songea, Ruvuma |
| 14. | Hebel M. Mwanisisi | Me | Mkulima | Iwindi | Iwindi | Iwindi Moravian Church<br>S. L. P. 1190 Mbeya |
| 15. | Lugano W. Mwandenga | Me | Mkulima | Chimala | Chimala | S. L. P. 78 Chimala-Mbarali |
| 16. | Fadhili M. Kitete | Me | Mkulima | Namtumbo | Namtumbo | S. L. P. 02 Namtumbo, Songea |
| 17. | Mary Seketea | Ke | Mkulima | Mbuza | Mkowe | S. L. P. 229 Sumbawanga |
| 18. | Sixberth N. Ndunguru | Me | Mgani (VEO) | Lilondo | Wino | S. L. P. 174 Songea, Ruvuma |
| 19. | Nictor Y. Ngusi | Me | Mgani (VEO) | Matai | Matai | Kilimo Wilaya<br>S. L. P. 232 Sumbawanga |
| 20. | Hassan J. M. S. Zayumba | Me | Mgani (VEO) | Idodi | Idodi | S. L. P. 290 Iringa |
| 21. | Peter J. Ndakidemi | Me | Mgani (VEO) | Chimala | Chimala | S. L. P. 141 Chimala |
| 22. | Meshack J. Mbogollo | Me | Mtafiti | ARI Uyole | ARI Uyole | ARI Uyole<br>S. L. P. 400 Mbeya |
| 23. | Anthony M. Elanga | Me | Mtafiti | ARI Uyole | ARI Uyole | ARI Uyole<br>S. L. P. 400 Mbeya |
| 24. | Zacharia J. U. Malley | Me | Mtafiti | ARI Uyole | ARI Uyole | ARI Uyole<br>S. L. P. 400 Mbeya |
| 25. | Dorothy Machunda Gimbi | Ke | Mtafiti | SUA | SUA | Idara ya Sayansi ya Chakula<br>S.L.P. 3006 Morogoro |
| 26. | Ephraim M. M. Senkondo | Me | Mtafiti | SUA | SUA | S. L. P. 3007 Morogoro |
| 27. | Nemes E. T. Makembe | Me | DALDO | Iringa | Iringa | S. L. P. 290 Iringa |
| 28 | Holiday A. Mwakasaka | Ke | NGO | Lizaboni | Lizaboni | S. L. P. 268 Songea |
| 29 | Filemon B. Mpwehwe | Me | DEO | Iringa | Iringa | S. L. P. 290 Iringa |
| 30 | Emil M. P. Kissoka | Me | Afisa Habari | Iringa | Iringa | Kitengo cha Habari (Uenezi)<br>S. L. P. 389 Iringa |
| 31 | Grete Benjaminsen | Ke | Mtafiti | ÅS Norway | ÅS Norway | S.L. P. 5001 Noragric, NLH |

| Na. | Jina | Jinsia | Kazi | Kijiji | Kata | Anuani |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Norway | 1432 ÅS, Norway |
| 32. | Dismas Mwaseba | Me | Mtafiti | SUA | SUA | Idara ya Elimu na Ushauri<br>S. L. P. 3000 Morogoro |
| 33. | Rogers E. Malimbwi | Me | Mtafiti | SUA | SUA | Idara ya Misitu<br>S. L. P. 3013 Morogoro |
| 34. | Akwilini J. P. Tarimo | Me | Mtafiti | SUA | SUA | Idara ya Mimea Vipando<br>S. L. P. 3005 Morogoro |
| 35. | Elimpaa Kiranga | Me | Mtafiti | ARI Uyole | ARI Uyole | ARI Uyole<br>S. L. P. 400 Mbeya |
| 36. | Joyce G. Lyimo-Macha | Ke | Mtafiti | SUA | SUA | Taasisi Elimu ya Kujiendeleza<br>S. L. P. 3044 Morogoro |
| 37. | Razack O. Msangi | Me | Facilitator COAS | Iringa | Iringa | C/O COAS<br>S. L. P. 664 Iringa |

**KIAMABATANISHO B**
**RATIBA**

| SAA | SIKU YA 1 | SIKU YA 2 | SIKU YA 3 |
|---|---|---|---|
| 2:30 asubuhi<br>↓<br>4:30 | • UTANGULIZI, MAMBO YA AWALI NA UFUNGUZI<br>• KUGAWANA MAJUKUMU (Viongozi)<br>• KANUNI ZETU<br>• MATARAJIO NA WASIWASI<br>• KUPANGA RATIBA | • TAARIFA FUPI MAMBO MUHIMU TULIYOJIFUNZA SIKU YA 1<br>• Mawasilisho ya matatizo kuendelea (vikundi 4) | • Tupo wapi sasa<br>• Mambo muhimu ya siku ya 2 (tumejifunza nini hadi sasa)<br>• Mapendekezo na wahusika (vikundi) |
| | C H A I | | |
| 5:00<br>↓<br>7:00 | • KUBAINI MATATIZO YA MASOKO YA MAZAO YA CHAKULA<br>- Kukubaliana maana ya maneno muhimu, Soko, Sokoni, Soko huria, tatizo na matatizo<br>- Kazi vikundini | • Majadiliano kukubalina matatizo<br>• Kubaini tatizo kuu | • Kuendelea kuwasilisha mikakati n.k.<br>• Kujadiliana<br>• Kufikia muafaka wa mikakati na wahusika wakuu<br>• Tathmini ya warsha |
| | CHAKULA CHA MCHANA | | |
| 8:30<br>↓<br>10:30 | - Kazi vikundini<br>- Kuanza kuwasilisha (matatizo) (vikundi 4)<br>- Je umejisikiaje leo? | • Kazi vikundini kuweka mikakati na kupendekeza wahusika<br>• Je umejisikiaje leo? | • Kufunga warsha |

## (KIAMBATANISHO C)

1. ZOEZI LA HESABU YA UMOJA –(Lengo 1 jawabu 1)


*Maelezo* - Kama wakulima wakishirikiana (wakishikamana) wakawa na dhamira moja, wakajipangia utaratibu (mfumo wao) wa kutatua matatizo yao – siku zote watapata majawabu yaliyo <u>SAWA</u> au yanayofanana. Mfano hizi namba 621, 532 na 853 zimetolewa na kujumlishwa (kufuata utaratibu fulani, nidhamu maalum) na kupata jawabu moja la 1089

| | | |
|---|---|---|
| 621 | 532 | 853 |
| -126 | -235 | -358 |
| 495 | 297 | 495 |
| +594 | +792 | +594 |
| 1089 | 1089 | 1089 |

**Jibu moja wote = <u>1089</u>.**

2. UTATU WA KUBORESHA MAHUSIANO (TARP II-SUA Project)

*Maelezo* - Kujenga na kuboresha mahusiano kati kati ya wakulima, wagani na watafiti siku zote KUTAZAA mahusiano mapya, kuona kupya (new vision) ubunifu mpya, uzalishaji wa kutosha na hivyo kuongeza kasi ya maendeleo........ uhakika wa chakula katika kaya utakuwepo na sekta ya kilimo na mifugo itaboreka kwa ujumla wake. Tuanze na kuiendeleza hii safari kwa kuvunja gamba la ubinafsi linalotutawala.



Hatua ya kwanza ya safari, ni kila mtu mshiriki/mdau wa Mradi wa TARP II-SUA atoke ndani mwake awezeshwe kutoka na kusema yanayomsibu na kupendekeza utatuzi (solutions). Wengi wanaushukuru Mradi kwa hilo-hii ni pamoja na sisi COAS. Kimsingi hakuna sababu za mradi huu kutofanikiwa – kutotoa matokeo (outputs) yaliyotegemewa. Kama zitakuwepo basi zitafahamika kisayansi.

**(KIAMBATANISHO D)**

***1. TUJITAMBUE SOTE – (DIRISHA LA JOHARI)***

***Maelezo***

Kila mtu ni kama fumbo lenye sehemu moja iliyo wazi na sehemu nyingine ambayo imefichika. Zoezi hili la dirisha la Johari (lililotungwa na Joe Luft na Harry Ingham) linatusaidia kuelewa jinsi ya kukua katika kujifahamu, na jinsi ya kujenga kuaminiana katika timu za watu na jamii tunamoishi kwa kushirikishana na kupeana mshindo nyuma au kukosoana. Wakulima, watafiti na wagani sote tunaweza kupanua sehemu yetu ya "UHURU" kwa kupunguza ukubwa wa sehemu za "UPOFU", "GIZA" NA "ILIYOJIFICHA" ili tujenge mahusiano bora, ya wazi na ya kweli wakati wote tutakuwa tunaendelea mbele

***Kielelezo cha Dirisha la Johari***

| | Inayojulikana kwa mwenyewe | Isiyojulikana kwa mwenyewe |
|---|---|---|
| Inayojulikana kwa wengine | **HURU**<br>- unaifahamu wewe<br>- wengine wanaifahamu | **KIPOFU**<br>(huijui)<br>(mshindo nyuma) |
| Isiyojulikana kwa wengine | **ILIYOFICHIKA**<br>-haijulikani na wengine (wewe tu) | **GIZA**<br>(akiba) |

Kushirikishana

(kufunua/kufumba_

**2. NYUSO MBILI (NJIA MBALIMBALI ZA KUANGALIA MATATIZO)**

Picha yenyewe yenye nyuso mbili haikuambatanishwa humu lakini nakala za kutosha ziligawanywa kwa washiriki na ufafanuzi kutolewa.

***Lengo*** – Lengo la zoezi hilo lilikuwa kuwafanya washiriki wa kongamano hilo kutambua njia mbalimbali za kukabiliana na matatizo kwa kushirikishana/kuonyeshana. Njia hii itawasaidia/iliwasaidia kutambua matatizo yao na kuyarekebisha, na kujenga hali ya mahusiano mazuri katika kikundi (jamii) ili waanze kushughulikia tatizo moja baada ya jingine kutegemeana na uzito wa tatizo na hali ya mahali.